## Mikakati ya NHBRA

NHBRA inaimarisha na kupanua wigo wa ushirikiano na jumuiya mbalimbali za kijamii (CBOs), Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs), Vyama vya Ushirika. Pia, Wizara, Idara na Wakala za Serikali, Wafadhili na Watu binafsi katika kutekeleza majukumu yake. Huduma na ufuatiliaji wa karibu unatolewa kuhakikisha kuwa huduma bora zinapatikana wakati wote.

Ili NHBRA ifanikiwe katika huduma zake ni muhimu: -

- Kuwa na matokeo ya utafiti juu ya makazi ya binadamu yanayopatikana kulingana na mahitaji ya wateja kwa muda unaotakiwa.
- Kuboresha mbinu za usambazaji wa matokeo ya tafiti hizo ili kuwafikia walengwa kwa wakati muafaka.
- Kutoa huduma bora za utafiti na ushauri.
- Kutoa huduma na vifaa bora na utaalam wa ujenzi ili kuwaridhisha washitiri na wadau.
- Kuongeza mapato ya Wakala.

## Mbinu za kusambaza matokeo ya utafiti na utaalam.

NHBRA imeandaa mikakati ya utekelezaji wa majukumu yake (strategic plan) kutokana na mchanganuo wa kibiashara (Business Analysis) kwa lengo la kutoa huduma safi na bora

Huduma mbalimbali za kitaalam hutolewa kwa njia zifuatazo:

- Utafiti na kutembelea wadau, washitiri na wateja ili kuhakiki mahitaji yao.
- Matangazo na makala katika vyombo vya habari.
- Kushiriki maonesho mbalimbali.
- Mbinu shirikishi za mafunzo kwa vitendo.
- Machapisho mbalimbali ya kitaalamu
- Kushiriki mikutano, warsha, semina na makongamano mbalimbali katika sekta. ya ujenzi
- Kukaribisha wanafunzi wa vyuo mbali mbali kwa mafunzo ya vitendo (practical training).
- Kuunda na kutoa mafunzo kwa vikundi vya ujenzi (Grassroot Building Brigades-GBBs) ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya vitakavyohusika na uzalishaji wa vifaa na ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu katika maeneo yao kwa lengo la kujiendesha vyenyewe kibiashara ili kukuza ajira hasa kwa vijana.
- Kuingia mikataba ya maelewano (Memorandum of Understanding and Service Level Agreements) na watu binafsi, makampuni, taasisi na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na jumuiya za kijamii (CBOs) za kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kutangaza na kusambaza teknolojia ya nyumba bora za gharama nafuu nchini kama mchango wa Wakala katika kuondoa umaskini Tanzania.

WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

NHBRA TANZANIA

# WAKALA WA TAIFA WA UTAFITI WA NYUMBA BORA NA VIFAA VYA UJENZI (NHBRA)




**Kwa mawasiliano zaidi:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**S.L.P 1964,**
**DAR ES SALAAM**

**Simu:** +255 022 2771971
+255 022 2774003
**Nukushi:** +255 022 2774003
**Mobile:** +255 762 462081
**Barua pepe:** dg@nhbra.go.tz

# Utangulizi:

Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi ulianzishwa kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Na..30 ya Mwaka 1997 kulingana na mageuzi ya mfumo wa utendaji kazi kiufanisi Serikalini.

### Madhumuni ya NHBRA

Madhumuni ya NHBRA ni kuwezesha wananchi wa Tanzania kufanikiwa kupata nyumba bora kwa kutumia rasilimali zipatikanazo hapa nchini na ufundi mahsusi ifikapo mwaka 2025.

### Majukumu ya NHBRA

Kutoa huduma za utafiti na vifaa bora kuhusiana na nyumba za gharama nafuu kwa lengo la kuinua kiwango cha ubora wa nyumba za kuishi na hivyo kuinua maisha ya watu wa mijini na vijijini kwa ujumla.

NHBRA inatoa na kusambaza teknolojia ya vifaa bora vya ujenzi, na ufundi ili:

- Kupata nyumba imara
- Kupata nyumba safi kwa afya ya binadamu.
- Kupata nyumba zenye ubora unaozingatia mila,desturi na heshima ya binadamu.

### Muundo wa NHBRA

NHBRA iko chini ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Wizara inasaidiwa na Bodi ya Ushauri (Ministerial Advisory Board). Wakala unaendesha shughuli zake za kila siku chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mkuu (Director General).

### NHBRA ina Idara tatu:-

- Idara ya Utafiti na Maendeleo (Research & Development )
- Idara ya Ushauri (Consultancy)
- Idara ya Biashara na Utawala (Business Support)



**Ofisi ya Mbunge-Manyoni**

### Kazi za NHBRA

Kulingana na Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, mhimili wa kazi za undani ya Muundo wake hapo juu.

M

hapo j

Kazi za NHBRA zinajumuisha utoaji wa huduma na vifaa kama ifuatavyo:

kama

(a)

#### a) Huduma zitolewazo:

- Kuendesha utafiti wa vifaa bora na ufundi wa ujenzi kwa lengo la kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba.
- Kuuza matokeo ya utafiti wa kitaalamu.
- Kutoa huduma ya ushauri, usanifu, ukadiriaji gharama za majenzi na usimamizi wa ujenzi wa nyumba.
- Kuendesha mafunzo na semina mbalimbali kuhusu nyumba za gharama nafuu zitumiazo maliasili zipatikanazo maeneo ya ujenzi.
- Kutoa huduma za uchongaji na ukataji wa vyuma ,mbao, vigae na vifaa vingine ndani ya karakana zake.
- Huduma za ujenzi, ukarabati na matengenezo ya nyumba
- Kutoa huduma ya maktaba maalum ya maendeleo ya nyumba bora.
- Kuishauri Wizara mama juu ya Sera ya Nyumba Bora na Makazi ya Binadamu.



Jengo la Shule ya Sekondari ya Sokoine-Mvomero



#### b) Baadhi ya Vifaa vipatikanavyo NHBRA.

- Mashine za kufyatua matofali yanayofungamana (interlocking bricks).
- Mashine za kutengeneza vigae bora vya kuezeka nyumba.
- Kalibu mbalimbali za vigae na matofali
- Matofali yanayofungamana.
- Matofali ya vyoo vilivyoboreshwa vya VIP.
- Samani bora za nyumbani.
- Madawati bora ya shule za msingi na sekondari.
- Majarida, ripoti za utafiti, miongozo ya kiufundi na vipeperushi.
- Ramani za nyumba bora.

### NHBRA iko wapi?

NHBRA iko barabara ya Sam Nujoma, karibu na kituo cha mabasi cha Mwenge, umbali wa mita 400 kutoka Barabara ya Ali Hassani Mwinyi kuelekea ubungo, kati ya Kambi ya JWTZ na kituo cha mafuta cha Oilcom, Wilayani Kinondoni.

